# The best insha
# KCPE 2006

Malizia kwa: Sherehe zilipomalizika nilirudi nyumbani nikiwa na furaha tele.

: ACHANIKAYE KWENYE MPINI HAFI NJAA.

Maswali mpururu yalinizunguka tamulini mwangu. "Ningefanyaje?" ndilo lililokuwa swali nyeti tafakurini mwangu. Wiki ijayo, kungekuwe mashindano ya langalanga yaani, mashindano ya mbio za magari.

Gari langu lilikuwa kweche, bovu kando. Sikuwa na hela zozote za kugharamia malipo ya kutengenezwa kwake. Niliwaza nikawazua lakini jambo hilo lilikuwa mathalan wingu la kitendawili lililonitandia, nami sikuweza kupata suluhisho. Ebo! Weledi wa lugha hawakuboboja maneno ovyo walipoamba, 'jambo usilolijua ni usiku wa giza.'

Kwa kuwa pasipo budi hubidi, niliamua kulitumia gari langu bovu kama ilivyokuwa.

Nikapiga moyo konde na kung'amua kuwa liwalo na liwe. Nimmelitumia gari hilo langu namna ilivyokuwa. "Bovu au zuri nitashinda!" nikajisemea.

Dakika zilipareji na kuwa saa, saa nazo zikavunja ungo na kuwa siku, vilevile siku zikabaleghe na kuwa juma. Naam, wazembwe na wazembwele hawakutupiga mlazamlaza walipokaa ukumbini, wakapiga alinacha na kuamba, hayawi hayawi huwa aidha hauchi hauchi hucha. Asubuhi ya mashindano ikafika.

Nilidamka macheo mbichi nikaziambua nyayo hadi uwanjani pa mashindano. Gari langu lilikuwa keshafika. Mwia si mwia, niliwasili. Nikayaona magari ya washindani wengine. Astaghafirullahi! Yalikuwa mazuri mno! Lo! "Je, ningeshinda?" nilijisaili huku jekejeke jembamba likinitoja na kunichuruzika chururu! Sikufa moyo asilani kwani wasemao husema, 'Mola hamtupi binadamu wake'.

Baada ya muda wa koo kumeza punje, nilifika ulingoni na kujitoma ndani ya gari langu. Nikajifunga mkanda na kusubiri kwa hamu na hamamu kipenga cha kuyaanzisha mashindano kipigwe. "Prrrr!" kikalia na magari yote yakataka shoti na kuacha kivumbi kikieleaelea hewani. Makofi ya kushangilia madereva yakaihinikiza hewa yote.

Magurudumu ya gari langu yalibugunya masafa kama vile kiwavi abugunyavyo jani dogo la ukoka. Nikajitahidi, mchwa kando na kuamini kuwa jitahada zangu zingezaa matunda. Waswahili walikuli, kuntu, mvumulivu nula mbivu.

Miwia ulipita, kukabaki kitalifa cha mita mia moja tu kuyamaliza mashindano. Nikazitumia nguvu zangu zote na kuibuka mshindi. Inna, mchumia juani hulia kivulini. Nilikuwa nimeshinda! Furaha ghaya ilinivamia vaa! nikachanua tabasamu sadakta kama tasa aliyekopoa mapacha. Makofi yalisikika kote kwa minajili ya kunisifu mimi. Ndipo nilipong'amua kuwa akina shekhe na manabodha wa jadi na jadadi hawakuvaa miwani ya mbao audha soksi za chuma walipolonga, mcheza kwao hutuzwa.

Nikaandaliwa sherehe maridhawa, sherehe ya kukata na choka. Nilituzwa kwa kuyashinda mashindano hayo. Nikabebwa halumbe halambe na mashabiki waliopenda uendeshaji wangu. Sherehe zilipomalizika nilirudi nyumbani nikiwa na furaha tele.

*(Alama iliyotuzwa 38)*

Insha hii ina mvuto mkubwa sana. Mtu akiisoma huzuia pumzi na kushusha anapomaliza. Mtahiniwa ni fundi wa uandishi kweli. Ameanza insha yake kwa kuandika vidokezo. Amepanga kazi yake vizuri katika aya. Ameakifisha insha vizuri na hati ni nadhifu. Ametumia semi vizuri wala hakuharibu kazi yake kwa semi zisizo na maana. Jumla ya makosa aliyofanya ni machache sana.

Mfano.

sarufi:

- ***Gari langu ilivyokuwa*** badala ya ***gari langu lilivyokuwa***
- Kutumia herufi ndogo badala ya kubwa.

## 4.3 MAPENDEKEZO KWA WALIMU

4.3.1 Ni vizuri mfundishe Kiswahili katika ujumla wake. Tafuteni vitabu ambavyo vimependekezwa na kuvitumia kufundishia.

4.3.2 Sisitizieni wanafunzi kuwa wakijibu maswali ya vifungu ni lazima wasome kifungu chote ili waweze kujibu maswali, wala wasijikite tu pale wanapofikiria kuwa swali limetoka.

4.3.3 Fundisheni kuwa maswali ya kifungu cha ufahamu ambayo hayaonekani kuwa na majibu moja kwa moja huulizwa katika mtihani. Wasaidieni kuzoea kujibu maswali ya aina hii. Maswali haya huweza kuwa ya stadi kama ya tathmini ambayo ni stadi ya juu katika zile stadi za ujuzi, ufahamu, matumizi, uchanganuzi, usanisi na tathmini.

4.3.4 Wanafunzi wenu ni lazima wasome kichwa cha insha na kuelewa mada na kutoa hoja nyingi. Si vizuri kutumia msamiati mkubwa ama mwingi mwingi ambao unapoteza maana iliyokusudiwa ama kutumika vibaya tu.

Compiled& distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel: +254734579299 E-mail: infosnkenya@gmail.com |

ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com